



Trent Park Elementary School

2500 Educational Drive, New Bern, NC 28562

Phone: 252-514-6481 Fax: 252-514-6485

www.trentparkelementary.com

Ashley Faulkenberry
Principal

Leslie Pope
Assistant Principal

Tarehe 25 Agosti 2025

Mpendwa Mzazi/Mlezi:

Shule ya mtoto wako hupokea fedha za Shirikisho kupitia mpango wa Title I ili kusaidia wanafunzi kufikia viwango vya mafanikio vya jimbo. Barua hii inakujulisha kuhusu haki yako ya kuomba taarifa kuhusu sifa za wafanyakazi wa darasani wanaomfundisha mtoto wako na taarifa kuhusu mitihani ambayo wanafunzi wanafanya wakati wa mwaka wa masomo.

Shule zinazoshiriki katika mpango wa Title I lazima zitimize kanuni za shirikisho zinazohusiana na sifa za walimu kama inavyoelezwa katika ESEA (Elementary and Secondary Education Act, Sheria ya Elimu ya Msingi na Sekondari). Kanuni hizi hukuruhusu kujua zaidi kuhusu mafunzo na vyeti vya walimu wa mtoto wako. Wakati wowote, unaweza kuuliza:

- Ikiwa mwalimu anakidhi masharti ya jimbo ya sifa na vyeti kwa kiwango cha gredi na somo analofundisha
- Ikiwa mwalimu amepata cheti cha dharura au maalum ambacho kilihitaji kuondolewa kwa masharti ya jimbo
- Mwalimu ana shahada gani za kwanza au za uzamili, na somo(masomo) au nyanja alizosomea.
- Ikiwa mtoto wako anapokea usaidizi kutoka kwa mtaalamu msaidizi, na ikiwa anapokea, sifa zake

Sheria ya Every Student Succeeds Act (ESSA, Kila Mwanafunzi Anapaswa Kufaulu) ambayo ilipitishwa kuwa sheria mnamo mwezi Desemba 2015 na kuidhinisha upya sheria ya ESEA, inajumuisha haki ya ziada ya mzazi kutuma maombi ya kujua, ikiwa na pamoja na kujua:

- Taarifa kuhusu sera za ushiriki wa wanafunzi katika mitihani na taratibu za kujiondoa kushiriki
- Taarifa kuhusu mitihani inayohitajika ikiwa ni pamoja na:
 - mada inayotahiniwa
 - kusudi la mtihani huo
 - chanzo cha masharti ya mtihani huo (ikiwa kipo)
 - muda ambao wanafunzi huchukua kumaliza mtihani
 - muda na muundo wa kutangaza matokeo

Taarifa zote zilizo hapo juu zinaweza kuombwa kupitia mwalimu mkuu wa shule yako.

Shule za Kaunti ya Craven zimejitolea kikamilifu kumsaidia mtoto wako kukuza maarifa na ujuzi unaohitajika ili kufanikiwa shuleni na maishani. Tunathamini usaidizi na ushirikiano wako tunapojitahidi kutoa elimu bora kwa mtoto wako.

Kwa dhati,

Ashley Faulkenberry
Mkuu wa shule
Trent Park Elementary



Trent Park Elementary School

2500 Educational Drive, New Bern, NC 28562

Phone: 252-514-6481 Fax: 252-514-6485

www.trentparkelementary.com

Ashley Faulkenberry
Principal

Leslie Pope
Assistant Principal